



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA

BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA

Tovuti: www.hlpc.go.tz



TANGAZO

**KUFUNGULIWA KWA DIRISHA LA MAOMBI YA USAJILI WA AWALI
(PROVISION REGISTRATION) KWA NJIA YA MTANDAO**

Baraza la Wataalam wa Maabara linachukuwa nafasi hii kuwajulisha Wataalamu wote wanaotarajia kufanya maombi ya Usajili wa awali (Provision Registration) kuwa dirisha la maombi ya Usajili litafunguliwa rasmi tarehe **28 Oktoba 2022** na litafungwa tarehe **01 Novemba 2022**.

Waombaji wote wanatakiwa kuzingatia maelekezo yafuatayo;

1. Maombi yote ya Usajili wa Awali (Provision Registration) yatafanyika kwa njia ya mtandao kupitia anwani hii hprs.moh.go.tz
2. Waombaji wote wanatakiwa kuambatanisha barua ya utambulisho kutoka chuoni, nakala ya vyeti vya taaluma na kuzaliwa. Kwa Wataalam waliosoma vyuo vya nje ya Tanzania wanatakiwa kuambatanisha barua/cheti ya utambuzi kutoka TCU/NACTE
3. Kwa waombaji wa usajili wa awali ngazi ya Shahada wanatakiwa kukamilisha zoezi la maombi ya usajili ndani ya muda ili baada ya kufungwa kwa dirisha la usajili waweze kufunguliwa dirisha la maombi ya utarajali (**Internship**)
4. Maombi ya usajili yataanza kufanyiwa kazi baada ya dirisha la Usajili kufungwa
5. Orodha ya majina ambayo vyeti vya usajili vimetengenezwa yatawekwa kwenye tovuti ya Baraza (hlpc.go.tz) na siku za kuchukua vyeti vya usajili ni Jumatano na Alhamisi ya kila wiki.

Upatapo tangazo hili mtaarifu mwenzako.

Imetolewa na

Msajili

Baraza la Wataalam wa Maabara

